JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
KITENGO CHA UTAFITI NA MAFUNZO

# CHUO CHA MAFUNZO YA UHIFADHI WA MALIASILI KWA JAMII LIKUYU SEKAMAGANGA

## TANGAZO LA KOZI ZA UTALII NA UONGOZAJI WATALII KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga ni miongoni mwa vyuo vilivyoko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Chuo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi na Mafunzo ya ufundi stadi nchini (NACTVET) kwa **usajili namba REG/SAT/046.**

Mkuu wa Chuo anapenda kuutangazia umma wa watanzania na waombaji wenye sifa kutuma maombi ya kujiunga na mafunzo ya kozi ya Utalii na Uongozaji watalii katika ngazi zifuatazo;

| NA. | NGAZI (LEVEL) | MUDA WA MAFUNZO | SIFA ZA KUJIUNGA | GHARAMA ZA MAFUNZO (TSH) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Astashahada ya awali ya Utalii na Uongozaji watalii – NTA level 4 | Mwaka mmoja (1) | i)Mhitimu wa kidato cha nne mwenye cheti chenye ufaulu usiopungua kiwango cha alama D kwa masomo manne isipokuwa masomo ya dini AU<br>ii) Mhitimu mwenye cheti cha "National Vocational Award (NVA) III" katika fani ya Utalii au Wanyamapori au Hoteli au Uongozaji watalii. Muombaji atakaye tumia cheti cha NVA III lazima awe amefaulu angalau masomo mawili (2) kidato cha nne. | **i) Ada: Tsh. 840,000/=**<br>**ii)Michango mingine: Tsh. 2,863,550/=** kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, malazi, chakula, huduma ya kwanza, cheti, sare na mahafali.<br>Malipo haya hulipwa kwa awamu mbili. |
| 2 | Astashahada ya Utalii na Uongozaji watalii – NTA level 5 | Mwaka mmoja (1) | i. Mhitimu wa kidato cha sita mwenye cheti chenye ufaulu usiopungua masomo mawili, ikiwemo "Principal pass plus one Subsidiary pass in Principal subjects" AU<br>ii. Mhitimu mwenye cheti cha "National Technical Award (NTA) level 4" katika fani za Utalii au Wanyamapori au Hoteli au Uongozaji watalii toka Chuo chochote kilichosajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi na Mafunzo ya ufundi stadi nchini (NACTVET). | **i) Ada: Tsh. 960,000/=**<br>**ii)Michango mingine: Tsh. 2,978,502/=** kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, malazi, chakula, huduma ya kwanza, cheti, sare na mahafali.<br>Malipo haya hulipwa kwa awamu mbili. |
| 3 | Stashahada ya Utalii na Uongozaji watalii – NTA level 6 | Mwaka mmoja (1) | Mhitimu mwenye cheti cha "National Technical Award (NTA) level 5" katika fani za Utalii na Uongozaji watalii au Wanyamapori au Hotel toka Chuo chochote kilichosajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi na Mafunzo ya ufundi stadi nchini (NACTVET). | **i) Ada: Tsh. 998,400/=**<br>**ii)Michango mingine: Tsh. 3,041,220/=** kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, malazi, chakula, huduma ya kwanza, cheti, sare na mahafali.<br>Malipo haya hulipwa kwa awamu mbili. |

### 1. TARATIBU ZA UOMBAJI:

i) Muombaji anatakiwa kujaza fomu ya maombi na kuiwasilisha kwa Mkuu wa Chuo baada ya kuambatanisha nakala za vyeti vyote vinavyotakiwa. Fomu za maombi zinapatikana chuoni au kwenye Tovuti ya Chuo www.cbctclikuyu.ac.tz

ii) Waombaji watachaguliwa kulingana na kigezo cha ufaulu wao.

### 2. TAFADHALI ZINGATIA YAFUATAYO:

i) Malipo yote yafanyike kupitia Namba ya malipo (Government control number) ambayo utapatiwa na Chuo.

ii) Waombaji wanatakiwa kulipa **ada ya maombi (application fee) shilingi elfu ishirini (20,000/=)** ambayo haitarudishwa. Ada ya maombi (application fee) inalipwa kupitia Namba ya malipo (Government control number) itakayotolewa na Chuo.

iii) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30 Septemba 2025.

**Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana na;**

**Mkuu wa Chuo,**
CBCTC-Likuyu Sekamaganga,
S.L.P 24,
Namtumbo, Ruvuma.
Simu za mkononi: 0754 352 846/0788 409 433,
Barua pepe: cbctc@maliasili.go.tz Tovuti: www.cbctclikuyu.ac.tz

**Afisa udahili,**
**Simu: 0738 102 111**